

Ukweli Wa Injili

MAFUNDISHO YA BIBLIA NA HIMIZO KWA
KAZI YA KIMISHENI ULIMWENGUNI KOTE

SANAMU KUU—UNABII WA DANIELI KUHUSU UFALME

"Hii ndiyo ile ndoto, nasi tutaihubiri tafsiri yake mbele ya mfalme" (Danieli 2:36). Hayo ndiyo maneno ambayo nabii Danieli alimwambia Mfame


Nebukadreza, mfalme ambaye alikuwa na nguvu na mamlaka mengi huko katika ufalme wa Babeli. Ufalme huu ndio ulikuwa mkuu zaidi kote duniani nyakati hiso. Nebukadreza alikuwa akisumbuliwa na ndoto ambayo hangeweza kuikumbuka vizuri. Lakini kuitia ufunuo kutoka kwa Mungu ambaa Danieli alitoa siri ya ndoto na maana yake ikafunuliwa.

Mfalme alikuwa ameota kuhusu sanamu kubwa ya mtu ambaye alikuwa amesimama mbele yake. Kichwa cha mtu huyo kilikuwa cha dhahabu safi; kifua chake na mikono yake ilikuwa ya fedha; tumbo lake na viuno vyake vya shaba; miguu yake ilikuwa ya chuma; na nyayo za miguu yake zilikuwa nusu chuma na nusu udongo. Ndipo Danieli akatoa maelezo kwamba sanamu hiyo iliwakilisha mfululizo wa falme nne ambazo zingesambaa kote duniani.

Kichwa ambacho kilikuwa cha dhahabu kilimwakilisha Nebukadreza na ufalme wake mkubwa huko Babeli. Ufalme huu ulikuwa ufalme wa kwanza mkuu, mkuu zaidi ya falme zingine zote ambazo zilisambaa kote duniani. Chanzo cha ufalme huo kilikuwa ufame wa kale wa Asiria ambaa ulianzishwa na Nimrodi.

Mfalme Nebukadreza akatawala katika ufalme huu wenye utajiri mkubwa kutoka 606 Kabla ya Kristo (KK) had 561 KK.

Naye Danieli akatabiri kuhusu kuanguka kwa ufalme huo wa Babeli na



kuzinduka kwa ufalme mkuu wa pili. Hapo mwaka wa 538 KK unabii huu ukatimia wakati Mfalme Dario Mmedi na Mfalme Mkuu Koreshi wa Uajemi walipoungana pamoja na kuangusha

ufalme wa Babeli (Danieli 5:31). Hapo ndipo kukazuka ufalme wa Wamedi-Wajemi ambaa uliwakilishwa na mikono na kifua cha fedha. Ufalme huu haukuwa mkuu kama ule wa Babeli.

Naye Aleksanda Mkuu akapindua ufalme wa Kijemini na akashinda ulimwengu wote wa siku hizo hapo mwaka wa 330 KK. Ndipo ufalme wa Kiyunani ambaa uliwakilishwa na tumbo na mapaja ya shaba ukaanzishwa. Aleksanda alipokufa ufalme wake ukagawanyika sehemu nne, kila moja ikitawaliwa na mmoja wa majemadari wake. Lakini ufalme huo uliendelea kuwa dhaifu na mwishowe ukaangushwa na Warumi hapo mwaka wa 146 KK.

Nao ufalme wa Kirumi ambaa pia ulikuwa ufalme wa mwisho ambaa ulisambaa kote ulimwenguni uliwakilishwa na miguu ya chuma. Nyayo zake ziliundwa kwa udongo na chuma zikiwakilisha ukosefu wa udhabiti wa kindani ambaa ulizinduka hapo baadaye wakati ambapo ufalme huo uligawanyika na kuwa falme kumi ndogo. Hakuna unabii mwingine ambaa umetolewa wa ufalme mwingine uliosambaa duniani kote.

Ni wakati ambapo ufalme wa Kirumi ulikuwa kileleni chake katika utawala wa

(Inaendelea kutoka ukurasa 2)

Tahariri

Ukurasa 3

Mwongozo wa Kujifunza
Biblia: Ufalme wa Mungu
Ukurasa 4
Jarida la Umoja
Kurasa 5-6

Unabii Kuhusu Ufalme

Ukurasa 7

S & J: Isaya 11
Inamaanisha Nini?

Kurasa 8-9

Je, Wajua?

Kuishi kwa Injili
Ukurasa 10

MAMBO AMBAYO

BIBLIA

Inafundisha Kuhusu...

Neno la Mungu

2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

Uhusiano wa Upendo

Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, I Yoh. 4:7-21

Toba

Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

Uzao Mpya

Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4, Efe. 2:1, 5-6

Uhuru Kutokana na Dhambi

I Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

Ujazo wa Roho Mtakatifu

Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

Utakatifu

Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, I Pet. 1:15-16,

Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

Ufalme wa Mungu

Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

Kanisa

Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, I Kor. 12:12-13,

Kol. 1:18

Umoja

Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

Kanuni za Kanisa

Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27,

Yn. 13:14-17

Uponyaji wa Kiungu

Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

Utakatifu wa Ndoa

Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3,

I Kor. 7:10-11

Urembo wa Nje

I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

Mwisho wa Nyakati

2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10, Mt.

25:31-46

Kupenda Amani

Lk. 6:27-29, 18:20

Ibada

Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

Wajibu Mkuu

Mk. 16:15

(Endelea kutoka ukurasa I)

Kaisari Augusto ndipo Yesu Kristo alizaliwa duniani. Nabii Danieli akatabiri na kusema, "Na katika siku za wafalme hao Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao hautaangamizwa milele . . . nao utasimama milele na milele" (Danieli 2:44).

Nebukadreza alikuwa ameota ndoto kuhusu jiwe lililokatwa kutoka mlimani bila kutumia mikono ya mwanadamu na ambalo lilivunjavunja sanamu hiyo. Jiwe hilo likasambaa ulimwenguni kote. Huu ndio unabii kuhusu Ufalme wa Mungu, Ufalme wa ajabu, Ufalme ulioanzishwa katika siku za wafalme hao. Yesu ndiye jiwe ambalo wajenzi walikataa lakini ambalo lilifanyika kuwa jiwa la pembedi (Matendo 4:11). Yeye alizaliwa na bikira na ufalme huo ulianzishwa wakati Yeye alikuja ulimwenguni kama mtoto mchanga. Kama ilivyotabiriwa katika kitabu cha Nabii Isaya, "Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa . . . na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake . . . maongeo ya enzi yake na amani hayatakuwa na mwisho kamwe" (Isaya 9:6-7).

Falme nne za kibinadamu ambazo zilisambaa kote ulimwenguni zilipata kuanguka moja baada ya nyingine. Lakini kuna ufalme ambao ulizinduka katika siku hizo ambao kamwe hautawahi kuangamizwa. Huu ndio ufalme wa ulimwengu wote, ufalme wa wa Yesu Kristo. Huu sio ufalme wa dunia hii, mbali ni ufalme wa kiroho, ufalme wa mbinguni, ambao hautafikia kikomo. Ujumbe wa injili umesambaa kote ulimwenguni. Serikali zilijaribu kuangamiza Ukristo lakini Ufalme wa Mungu uliendelea kusambaa.

Watu wengi wanaendela kusubiri Ufalme wa Mungu utakaokuja duniani humu, lakini ng'o hawataupata. Ufalme wa Mungu upo hapa, sasa hivi. Ufalme huo ulifika hapa duniani wakati Yesu alikuja mara ya kwanza, na hatuna haja ya kutafuta kufika kwake katika enzi nyingine. Leo ndio siku ya wokovu, na sasa ndio wakati ambao tunaweza kuingia katika amani, faraja, na baraka zote za Ufalme wa Mungu.

—mws

UKWELI WA INJILI

Gazeti la 'Ukweli wa Injili' huchapishwa kwa jina la Bwana kwa matumizi ya watu wa mataifa yote kwa kwa kusudi la kuimarisha na kuwashimiza watu wote katika ukweli wa neno la Mungu. Gazeti hili hufundisha na kueneza ukweli wa Biblia ambao umethitishwa tangu nyakati za Yesu Kristo na mitume.

Neno la Mungu ndio mwongozo halisi na wa kipekee wa imani. Linafundisha wokovu na ukombozi kutokana na dhambi unaotewa na utakaso wa Yesu Kristo; ambao hufuatiwa na ujazo wa Roho Mtakatifu anayemwongoza mhudumu, kumwonyesha njia, na kumpatia nguvu; pia unamletea mtu utakatifu halisi katika kila fani ya maisha yake; na pia kuleta umoja na utangamano wa watu wa Mungu. Huduma inayokubalika na Mungu inatokana na mtu kuwa na uhusiano wa kibinasi na wa upendo ambao msingi wake ni ukweli.

Waandishi: Michael na René Smith

UAGIZAJI

Ukweli wa Injili ni gazeti la kieletroniki linalochapishwa kila robo ya mwaka kwa jinsi Mungu anavyotuongoz. Tutembelee katika tovuti yetu ya www.thegospeltruth.org ili uagize jalida hili kupitia kwa orodha yetu ya anwani pepe na upokee toleo lako la wakati huu. Hebu jisikie huru kututumia orodha ya majina na anwani pepe za watu wengine ambao wangependa kupokea toleo hili kutoka kwa mwandishi wa jalida la Ukweli wa Injili.

WASILIANA NASI

Gazeti a Ukweli wa injili linachapishwa katika mataifa mbalimbali ili kusambazwa katika maeneo hayo. Kazi hii na zingine za kimishenari ambazo sisi hufanya huwezekana kupitia kwa matoleo ya kujitolea yanayotolewa kwa jina la Kanisa la Mungu.

Tahariri



Msiogope, enyi kundi dogo; kwa kuwa Baba yenu ameona vema kuwapa ule ufalme —Luka 12:32.

Mimi niliandika toleo hili la *Jalida la Ukweli* nikiwa na shukrani nyingi moyoni. Miezi hii michache iliyopita nimepitia mabonde yeny kina kirefu ambayo mimi kamwe sijawahi pitia maishani. Kuna bwana mmoja ambaye alishawahidi kuniambia kwamba, mwanadamu aidha atateseka na Bwana au atateseka peke yake. Mimi namshukuru Mungu kwa ajili ya nafasi ya kuteseka pamoja na Mwokozi wangu. Katika majaribu na dhoruba za maisha haya hakuna usalama ambao unaweza kushinda usalama wa mtu kuwa mikononi mwa Mwokozi wake. Kuna masumbufo mengi na mambo mengine magumu ambayo humjia mwanadamu katika maisha haya, lakini uwepo wa Mungu ndio humpa mwanadamu nguvu na ujasiri wa kukabiliana na siku nyingine maishani mwake. Ndiposa mimi naweza kusema pamoja na Ayubu "Mwokozi wangu yuaishi." Basi kwa kila mwiba na mjambe wa Shetani ambaye anatuandama kuna baraka nyingi zaidi na malaika wa mwanga ambao watasimama pamoja nasi na kutuunga mkono na hata kutuonyesha upendo. Mimi najisikia kuwa nimebarikiwa sana kwa kuwa mwananchi wa Ufalme wa Mungu. Na katika toleo hili la jalida la ukweli mimi nashiriki baadhi ya kweli hizo za ajabu za ufalme wa Mungu. Wakati mtu mtu anaingia katika nchi za kigeni, au wakati anarudi nchini mwao anatakiwa kuonyesha pasi ya usafiri. Pasi hii huonyesha utaifa wake, alikozaliwa n.k. Hata ingawa sote tuna utaifa wa nchi na serikali tofauti duniani, kila mtoto wa Mungu ana utaifa wa Ufalme wa Mungu. Utaifa huo unazidi baraka yote ya nchi zetu za kidunia. Wakati mtu amezaliwa tena na kuoshwa kwa damu ya Yesu Kristo yeye anafanyika kuwa sehemu ya jambo lililo kuu zaidi kuliko ufalme wa kidunia. Ndiposa mimi najihisi kubarikiwa sana kwa kuwa sehemu ya Ufalme wa Mungu.

Sina nafasi ya kusema kwa mapana na marefu kuhusu urembo na ukweli wa ajabu wa ukamilifu wa Ufalme wa Mungu. Ombi langu ni kwamba Roho Mtakatifu atachukua yote ambayo yamesemwa kwenye jalida hili na kuyafanya kuwa maradufu katika roho ya wasomaji wangu. Watu wengi wanamtazamia Kristo aanzishe ufalme wa kidunia, ambako kutakuwa na amani na utoshelevu wa mambo yote. Lakini mimi napata ujuzi wa kuwa na ufalme huu hapa hapa duniani, sasa hivi. Hata ingawa mtu wa nje anaendelea kudhoofika, mtu wa ndani anaendelea kufanywa upya. Mimi ni sehemu ya ufalme wa kiroho ambao kamwe hauwezi kuangamizwa. Kwa kweli kutakuwa na majaribu, lakini milango ya kuzimu haiwezi kushinda Ufalme huu wa Mungu. Katu siwezi kubadilisha baraka za utaifa huo kwa sababu ya utajiri na heshima zote za kilimwengu.

Basi hebu tuendelee kuwa watu wa kweli na walio waaminifu kwa Bwana na Mfalme wetu. Ndani yake kuna amani ambayo mwanadamu hawezu kuielewa. Lakini wakati nikiendelea kufurahia baraka za ufalme huo nitaendelea kutazamia sana kutimia kwa Ufalme wa Mbinguni ambao utakuwa wa milele.

Michael W. Smith

Apri 2013

mengi kwa
MTANDAO

Tutembelee kwa
www.thegospeltruth.org

ili uagize na kusoma
Jarida letu.



JE, IMANI YA MTU KUHUSU UFALME WA MUNGU NI JAMBO LILIO MUHIMU?

"Wewe amini unayotaka kuamini, mimi nitaamini ninayotaka kuamini—sote twaelekeea mahali moja na mafundisho ya kidini silo jambo muhimu." Hivyo ndivyo anavyosema Mkristo anayeunga mkono dini zote.

Lakini hili si jambo ambalo lina ukweli ndani yake kwa sababu kuna ukweli ambao unalingana na Biblia bila kuzingatia maoni ya makanisa tofauti au thiolojia.

Mafundisho ya kweli yanayosema kwamba Ufalme wa Mungu ni ufalme wa kiroho ni mafundisho yaliyo muhimu. Watu wakielewa jambo hili vizuri wataweza kumtafuta Mungu ili jambo hili liwe la kweli maishani mwao kwa wakati huu badala ya wao kutafuta utimilifu wa Ufalme wa Mungu katika siku sijazo, jambo ambalo halitawahi kuwa.

Katika mafundisho ya watu ambao wanaamini kwamba kutakuwa na ufalme wa kidunia wa Yesu, wakati mwingi wao wanafundisha kwamba wenye dhambi watapata nafasi nyingine ya kuokoka katika kipindi (hicho) kijacho. Lakini kipindi hicho hakitatwahi kuweko kwa maana "Leo ndio siku ya wokovu."

MWONGOZO WA KUJIFUNZA BIBLIA

SOMO: UFALME WA MUNGU

Somo la Biblia: *Tazama, utachukua mimba na kuzaa mtoto mwanamume; na jina lake utamwita Yesu. Huyo atakuwa mkuu, ataitwa Mwana wa Aliye juu, na Bwana Mungu atampa kiti cha enzi cha Daudi, baba yake. Ataimiliki nyumba ya Yakobo hata milele, na ufalme wake utakuwa hauna mwisho – 1 Yohana 4:16-70.*

Muhstasari: Ufalme wa Mungu sio ufalme wa kidunia ambao utaanzishwa hapo baadaye; ufalme wa Mungu ni ufalme wa wa kiroho ambao msingi wake uko miyoni mwetu kupitia kwa Yesu Kristo.

I. Ufalme huo unapatikana wapi?

- A. Yohana 18:36-37 Sio wa ulimwengu huu.
- B. Luka 17:20-21 Uko ndani yako.

II. Ni Ufalme wa Kiroho

- A. Warumi 14:17 Haki, amani na furaha.
- B. 1 Wakorintho 4:20 Ufalme unakuja kwa nguvu.

III. Wakati wa Kuanzishwa kwa Ufalme wa Mungu

- A. Luka 16:16 Mahubiri kuhusu ufalme huo yalianzishwa na Yohana Mbatizaji.
- B. Luka 4:43 Yesu alihubiri ufalme wa Mungu.
- C. Marko 1:14-15 Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia.
- D. Marko 9:1 Uliahidiwa kwamba utafika kabla ya wanafunzi kuaga dunia.
- E. Matendo 1:1-3 Ahadi hiyo ilitimia kwa kuja kwa Roho Mtakatifu.

IV. Kuingia katika Ufalme wa Mungu

- A. Yohana 3:3 Lazima mtu azaliwe mara ya pili.
- B. Luka 16:16 Jiingize kwa nguvu.

V. Utawala katika Ufalme wa Mungu

- A. Ufunuo 1:5-6 Ametufanya kuwa wafalme na makuhani.
- B. 1 Petro 2:9-10 Mzao mteule, taifa takatifu.
- C. Warumi 6:14-15 Nguvu za kushinda dhambi.
- D. 1 Yohana 5:4 Nguvu za kushinda ulimwengu.
- E. Ufunuo 15:2-3 Ushindi juu ya dini sisizo za kweli.
- F. Luka 20:17-20 Nguvu za kumshinda Ibilisi.

VI. Ushahidi kwamba Ufalme wa Mungu Tayari Umeanzishwa

- A. Waebrania 12:28 Tunapokea Ufalme.
- B. Wakolosai 1:12-13 Ametuhamisha na kutuingiza katika ufalme.
- C. Ufunuo 1:9 Yohana alikuwa katika ufalme.

VII. Kudumu kwa Ufalme

- A. Isaya 9:6-7 Kudumu milele.
- B. Danieli 2:44 Hautaangamizwa.

Himizo

Luka 12:31-32 Bali utafuteni ufalme wa Mungu, na hayo mtaongezewa. Msiogope, enyi kundi dogo; kwa kuwa Baba yenu ameona vema kuwapa ule ufalme.

UFALME WA MUNGU

Jarida la Umoja kwa Uchambuzi wa Biblia

WAYAHUDI WALITAFUTA UHURU WA KISIASA

Wayahudi amba walikuwa chini ya utawala wa serikali ya Kirumi walikuwa wakimtafuta Mesiya amba angekuja kukomboa taifa lao kwa njia ya kisiasa na kuanzisha ufalme wake. Wao walisoma unabii kuhusu wakati Mwana wa Mungu angetawala kwa mamlaka makubwa, wakati kungekuwa na amani, uponyaji, na ukombozi. Kabla ya wanafunzi kupata Roho Mtakatifu wao pia wakamuuliza Kristo, "Bwana, wakati huu ndipo unapowerudishia Israeli ufalme?" (Matendo 1:6). Wayahudi walimkataa Kristo kama Mwana wa Mungu kwa sababu hawakurejeshewa ufalme wao wa kidunia. Wao, pamoja na watu wengi wengine amba hujita Wakristo hutazamia siku za usoni wakati Mesiya atakuja na kuanzisha ufalme wake hapa duniani. Lakini ng'o, siku hiyo haitafika. Kwa njia ya wazi kabisa Neno la Mungu linafundisha kwamba Ufalme wa Mungu ulianzishwa wakati Yesu Kristo alikuja mara ya kwanza duniani. Basi watu amba wanashubiri siku itakayokuja hukosa furaha ya kububujika moyoni ambayo huletwa na Ufalme wa Mungu amba tuko nao sasa hapa duniani.

UFALME WA MUNGU SIO WA KIMWILI

Yesu alijua kwamba watu walikuwa wanangojea kupata Mesiya ambaangeanzisha ufalme unao-onekana hapa duniani. Ndiposa kabla ya Yeye kusulubiwa alinena kwa njia ya wazi na Pilato na kumwambia kwamba, "Ufalme wangu sio wa ulimwengu huu. Kama ufalme wangu ungekuwa wa ulimwengu huu, watumishi wangu wangenipigania . . ." (Yohana 18:36). Kwa kweli maandiko yako kinyume na mafundisho kwamba Ufalme wa Mungu ni wa kidunia. Mafarisayo nao walitaka kujuu kutoka kwa Yesu wakati Ufalme wa Mungu ungekuja. Naye Yesu akawajibu, "Ufalme wa Mungu hauji kwa kuuchunguza; . . . tazama, ufalme wa Mungu umo ndani yenu" (Luka 17:20-21). Ufalme wa Mungu sio serikali ya kisiasa ambayo imeshika uongozi wa kidunia wala ufalme huo hauna mfalme wa kidunia.



"Wakati umetimia na ufalme wa mungu umekaribia. Tubuni na kualni Injili."

Marko 1:15

UFALME WENYEWE NI WA KIROHO

Ufalme wa Mungu ni wa kiroho na unapatikana katika moyo wa kila mtoto wa Mungu. Ufalme wenyewe ni haki, amani na furaha ambayo inafanya kazi katika maisha ya muumini (Warumi 14:17). Amani ya kweli haipatikani kutokana na hali za nje ama kutokana na serikali yoyote ile, bali hupatikana kutokana na kazi ya Mungu moyoni mwa mwanadamu. Ndiposa Yesu akasema, "Amani nawaachieni; amani yangu nawapa; niwapavyo mimi sivyo kama ulimwengu utoavyo . . ." (Yohana 14:27).

UFALME HUO ULIANZISHWA NA YESU

Yohana Mbatizaji alianza kuhubiri ujumbe kuhusu Ufalme kwa kuwaambia watu kutubu, "Torati na manabii vilikuwapo mpaka Yohana; tangu wakati huo habari njema ya ufalme wa Mungu hutangazwa, na kila mtu hujiingiza kwa nguvu" (Luka 16:16). Naye Yesu akafundisha kwa njia ya wazi kwamba, "Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia. Tubuni na kuiamini Habari Njema!" (Marko 1:15). Ufalme huo haukuwa utimie katika siku zitakazokuja bali ulianzishwa

kupitia kwa Kristo; "Kweli nawaambieni, wako wengine papa hapa amba hawatakufa kabla ya kuuona ufalme wa Mungu ukija kwa enzi" (Mariko 9:1).

JE, TWAINGIAJE KATIKA UFALME HUO

Yesu akamwambia Nikodemo, "Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawesi kuuona ufalme wa Mungu" (Yohana 3:3). Mtu huingia ufalme huo anapotubu dhambi zake na kumruhusu Yesu kuwa mfalme wa maisha yake. Nguvu za ufalme huo zilitolewa katika siku ya Pentekoste wakati Roho Mtakatifu alijazwa moyoni mwa waumini (Matendo 2). Ukamilifu wa ufalme wa Mungu hupatikana kupitia kwa kipawa cha Roho Mtakatifu ambaye humpatia muumini nguvu, amani, furaha, uongozi, na utakatifu.

UTAWALA KATIKA UFALME WA MUNGU

Yesu amefanya tuwe "ufalme, na makuhani kwa Mungu, naye

(Endelea kwa ukurasa 6)

(Endelea kutoka ukurasa 5)

ni Baba yake . . ." (Ufunuo 1:6). Wakristo walioko kwenye ufalme huu wa kiroho hutawala juu ya dhambi, ubinafsi, ulimwengu na hata juu ya dini za uongo. Hadi sasa Kristo ndiye mfalme mwenye nguvu zote na ambaye anatawala kanisa lake (Wakolosai 1:18) na kuandika sheria yake miyoni mwa waumini. Yeye huwakomboa na kuwaponya na hata kuwatakasa.

MILANGO IMO WAZI KWA WATU WOTE KUINGIA

Ufalme tayari umeanzishwa na watu wote wanaweza kuingia ndani kupitia kwa Yesu Kristo. "Basi kwa kuwa tunapokea ufalme usioweza kutetemeshwa, na muwe na neema, ambayo kwa hiyo tumtolee Mungu ibada ya kumpendeza, pamoja na unyenyekevu na kicho" (Waebrania 12:28). Ufalme huo ultabiriwa kwa njia ya

unabii na kukamilika kupitia kwa kuja kwa Yesu Kristo kwa mara ya kwanza. Ufalme wenyewe hautakuwa na mwisho bali utadumu milele (Isaya 9:6-7).

Zingatia kwamba: Yesu

*atakaporudi mara ya pili atakuja
kuwaleta watu wote mbele ya
kiti cha hukumu cha Mungu.*

*Ulimwengu huu wa sasa
utaangamizwa (2 Petro 3:10-12).*

*Watakatifu nao wataingia
mbinguni na wale wasio*

*watakatifu watakuwa huko jehanamu milele. Tutasoma kuhusu
swala hili katika toleo linalofuata la Ukweli wa Injili.*



— mws

MAMBO YALIYO MUHIMU KATIKA KUANZILISHWA NA KUDUMISHWA KWA UFALME WA MUNGU

Muhstasari wa maandishi ya



1992 ya mwandishi H.M. Riggle

1. KIONGOZI NI MFALME

Mathayo 21:4-5 Tazama, mfalme wako anakuja kwako . . .

Wakolosai 1:18 Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa; naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote.

2. KITI CHA ENZI CHA MFALME CHA KUTOA MWONGOZO KWA UFALME WAKE

Waebrania 1:8 Lakini kwa habari za Mwana asema, kiti chako cha enzi, Mungu, ni cha milele na milele; na fimbo ya ufalme wako ni fimbo ya adili.

Waebrania 4:16 Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.

3. ENEO AMBALO MFALME ANATAWALA

Mathayo 28:18 Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani.

4. WATU AMBAO MFALME ANATAWALA

Yakobo 4:7 Basi mtiini Mungu.

1 Petro 3:22 Naye yupo mkono wa kuume wa Mungu, amekwenda zake mbinguni, malaika na enzi na nguvu zikiisha kutiishwa chini yake.

5. SHERIA YA KUONGOZA WANANCHI WA UFALME WAKE

Waebrania 8:10 . . . Nitawapa sheria zangu katika nia zao, na katika miyoyo yao nitaziandika; nami nitakuwa Mungu kwoo, nao watakuwa watu wangu.

TAMATI

Mambo haya yote muhimu yamo na yanafanya kazi katika kipindi hiki cha neema. Yesu Kristo ni Mfalme wa mbingu na nchi na anadumu kati ya watu wake. Yeye hukaa kwenye kiti chake cha enzi na Yeye ndiye kichwa cha kanisa. Sheria yake ya utakatifu imo miyoni mwa watakatifu wake na wao huwa na furaha yake katika maisha haya tunayoishi. Hii ndiyo sababu inatufanya tuseme kwamba tayari ufalme wa Mungu ushaanzishwa!



UFALME WA MUNGU

...na kutimizwa kwake

Unabaii

Kutimizwa Kwake

Isaya 2:2-4 Nyumba ya Bwana inafanywa imara.
(Mika 4:1-7)

Waebraania 12:22-23 Mmeufikilia mlima Sayuni.

Zaburi 2:6-9 Ufalme wa Mwana.

Matendo 13:33 Yesu afufuliwa.

Zaburi 110:1-3 Bwana atawala kutoka Sayuni.

Matendo 2:30,32-36 Yesu amekaa kwenye kiti chake cha enzi.

Danieli 7:14 Ufalme wenyewe mamlaka na utukufu.

Waefeso 1:20-22 Kristo ana mamlaka na nguvu zote.

Isaya 35:5-6 Magonjwa na maradhi yatataponya.

Mathayo 4:23-24; 8:16-17 Yesu aliponya magonjwa yote.

Isaya 35:6-7 Nyika zitabadilishwa.

Yohana 4:14 Yesu atoa maji yenyeye uzima.
Yohana 6:35 Kamwe hawatapatwa na njaa au kiu.

Mika 4:3-4 Amani isiyo na kifani.

Yohana 14:27 Yesu awapa amani.



Bali ninyi mmeufikilia

mlima Sayuni,

na mji wa Mungu

aliye hai.

MASWALI na MAJIBU

SWALI: KATIKA ISAYA 11 NI NINI MAANA YA WANYAMA WA PORINI KUDUMU PAMOJA KWA AMANI?

JIBU: Hebu tutazame andiko hilo: "Mbwa -mwitu atakaa pamoja na mwana-kondoo, na chui atalala pamoja na mwana-mbuzi; ndama na mwana-simba na kinono watakuwa pamoja, na mtoto mdogo atawaongoza. Ng'ombe na dubu watalisha pamoja; watoto wao watalala pamoja; na simba atakula majani kama ng'ombe. Na mtoto anyonyaye atacheza penye tundu la nyoka, na mtoto aliyeachishwa atatia mkono wake katika pango la fira" (Isaya 11:6-8).

Hili ni swali muhimu ambalo linafaa. Hii ni kwa sababu kuna michoro mingi ambayo huchorwa kufafanua andiko hilo ambayo huonyesha simba akilala na ndama, lengo la michoro hiyo likiwa kudhihirisha utawala wa miaka elfu moja humu duniani wakati Kristo ataanzisha ufalme wa kidunia. Lakini hii ni tafsiri ya Maandiko ambayo haifai na ambayo hailingani na maandiko

ambayo yanapatikana katika sura hii Isaya 11. Watu wamewaza na kuwazua kuhusu kipindi hicho ambacho kitakuja wakati ambapo kutakuwa na amani ulimwenguni kote na hata kukosekane matumizi ya mabavu (hata) kati ya wanyama. Wanadamu wametumia michoro ya ajabu na maneno matamu matamu kuonyesha kipindi hicho cha utukufu wa dunia.

Lakini Yesu alifundisha kwamba Ufalme wa Mungu ni ufalme wa kiroho, na sio ufalme wa kidunia. Basi Isaya 11 ni unabii mzuri wa kiishara kuhusu amani na umaja wa kiwango cha ajabu ambao hutokana na wokovu wa Yesu Kristo. Hatuna haja ya kutazamia siku zijazo ili



"Wanyama wanaotajwa hapa sio wale wa kawaida bali ni tabia za kinyama ambazo zinapatikana kati ya wanadamu."

kupata utimilifu wa unabii huo kwa maana unabii huoulitimia wakati Masiya aliquja ulimwenguni mara ya kwanza.

Hebu tutazame aya zinazozunguka maandiko hayo ili tuweze kupata

muktadha wa unabii huo: "Basi litatoka chipukizi katika shina la Yese, na tawi litakalotoka katika mizizi yake litazaa matunda" (Isaya 11:1). Aya hii na zile ambazo zinafuata zinaonyesha kwamba maandiko haya yanena kuhusu Kristo mwenyewe ambaye alitokana na uzaa wa Yese, babake Daudi, "Na itakuwa katika siku hiyo, shina la Yese lisimamalo kuwa ishara kwa kabilia za watu, yeze ndiye ambaye mataifa watamtafuta; na mahali pake pa kupumzikia patakuwa na utukufu" (Isaya 11:10). Andiko hili pia lanena kuhusu Yesu, kama pia linenavyo andiko la Yeremia 23:5 na Ufunuo 5:5 ambapo inasema, "Simba aliye wa kabilia Yuda, Shina la Daudi, yeze ameshinda . . ."

Mtume Paulo anazungumzia Isaya 11 na kujulisha wasomi wake kwamba andiko hilo limetimia kuptitia kwa Kristo. Kuhusu Yesu mtume Paulo anasema: "Kwa hiyo nitakushukuru kati ya Mataifa, nami nitaliimbia jina lako. Na tena anena, furahini, mataifa, pamoja na watu wake. Na tena, enyi mataifa yote, msifuni Bwana; enyi watu wote, mhimidini. Na tena Isaya anena, litakuwako shina la Yese, naye aondokeaye kuwatawala Mataifa; ndiye Mataifa watakayemtumaini. Basi Mungu wa tumaini na awajaze ninyi furaha yote na amani katika kuamini, mpate kuzidi sana kuwa na tumaini, katika nguvu za Roho Mtakatifu." (Warumi 15:8-13). Mtume huyu aliquwa akitoa mwongozo kwa kanisa la Rumi ili waweze kuwakubali waumini wa kutoka kwa Mataifa, ambao

walikuwa wameingia kwenye Ufalme wa Mungu kuititia kwa Roho Mtakatifu. Yesu alikuwa ameinuliwa kuititia kwa msalaba na kwa kufu na kufufuka kwake wanadamu wote walikuwa wamepata mweke wa kupata manufaa yote ya Ufalme wa Mungu. Yeye alikuwa sasa ni mtawala, sio tu katika maisha ya Wakristo waliokuwa Wayahudi bali pia katika maisha ya Wakristo wa nchi za Kimataifa; "Alikuja kwake, wala walio wake hawakumpokea. Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake" (Yohana 1:11-12).

Pumziko lenye utukufu ambalo linazungumziwa katika Isaya 11:10 lilitangulizwa kwa waumini katika wakati wa Kristo. Ujumbe wa Masiya ulisema kwamba, "Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha" (Mathayo 11:28). Unabii huo kuhusu pumziko la ajabu na amani yake linaashiria kwa njia ya moja kwa moja kwa amani ile ambayo Yesu alileta duniani. Hii ndiyo sababu wakati Yesu alizaliwa humu duniani malaika walitangaza, "Atukuzwe Mungu juu mbinguni, na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia" (Luka 2:14).

Kwa sababu tayari tushaeleza muktadha wa maandiko hayo tunaweza sasa kuanza kuyatafsiri. Kwa kweli tunajua kwamba hatuna haja ya kutazamia siku zijazo bali tunahitaji kutazama siku zilizopita na zilizomo ili tuweze kuelewa maana ya wanyama wa mwitu kuishi kwa umoja. Ni dhahiri kwamba hadi sasa wanyama bado hawaishi kwa njia iliyoelezwa hapa. Ndiposa tunastahili kukumbuka kwamba ufalme wa Mungu ni wa kiroho na kwamba pumziko hilo na amani hiyo ilikuwako na ingaliko hadi sasa kati ya watoto wa kweli wa Mungu. Basi tunastahiri kuelewa andiko hilo kwa njia ya kiroho. Ni dhahiri kwamba wakati mwangi unabii hutolewa kwa njia ya

kiishara na ndivyo ilivyo katika andiko hilo la Isaya 11. Wanyama wanaotajwa hapa sio wale wa kawaida bali ni tabia za kinyama ambazo zinapatikana kati ya wanadamu. Unabii wa aina hiyo ni jambo la kawaida sio tu katika Agano la Kale bali pia katika Agano Jipy. Nabii Ezekieli alisema, "Wakuu wake kati yake wamekuwa kama mbwamwitu wakirarua mawindo; ili kumwaga damu, . . ." (Ezekieli 22:27). Naye Yesu akawaambia wanafunzi wake, "Enendeni, angalieni, nawatuma kama wana kondoo kati ya mbwamwitu" (Luka 10:3). Pia Yesu akinena



Basi Isaya 11:6-8 ni hadithi ya watu ambao kwa kawaida wangekuwa maadui lakini sasa wakiishi kwa amani mmoja na mwengine . . . watu wadhaifu na wenye nguvu . . . wakiishi pamoja kwa utulivu"

kumhusu Herode alisema kwamba, "Nendeni, mkamwambie yule mbweha" (Luka 13:32). Watu hao ambao wametajwa hapa walikuwa wakidhihirisha sifa za wanyama hao. Mbwa mwitu wanaotajwa hapa waliwakilisha watu ambao walikuwa tayari kuangamiza wale wengine. Wana kondoo nao hudhihirisha tabia za

unyenyekevu na utifu. Nao mbweha waliwakilisha mtu mwenye hila na udanganyifu.

Basi Isaya 11:6-8 ni hadithi ya watu ambao ingawa kwa kawaida wangekuwa maadui lakini sasa wakiishi kwa amani mmoja na mwengine. Jambo hili linawakilisha hali ya maelewano ya kustajabisha kati ya watu wa tabaka, sifa na hulka tofauti tofauti. Watu ambao kwa kawaida hawangekuwa na usalama wakiishi kwa maelewano na wale ambao kwa kawaida huwa na uwezo wa kuwaangamiza watu wale wengine. Watu wadhaifu na wenye nguvu, wanaoishi mwituni na wa kinyumbani, wenye kuleta madhara kwa watu wale wengine, na wasioleta madhara, wote wakiishi pamoja kwa utulivu. Je, jambo hili lawezekanaje? Jambo hilo haliwezekani tu, bali pia ni jambo la kawaida katika Ufalme wa Mungu. Watu wa mataifa tofauti na hulka tofauti huingia kwenye Ufalme wa Mungu kuititia kwa Yesu Kristo. Utu wao wa kale hubadilishwa na mambo yote kufanya kuwa mapya (2 Wakorintho 5:17). Katika siku zetu wana wa Mungu chini ya uongozi na utawala wa Masiya wana usalama na umoja. Sasa wamekuwa watu wa kushiriki sifa za kiungu (2 Petro 1:4), na zile sifa za kale za ukali, uadui na kimwili zinabadilishwa na kuwa sifa za upendo na amani. Je, si ni jambo la ajabu mtu kuwa mshirika wa Ufalme wa Mungu katika siku zetu? Basi Isaya 11:6-8 ni mchoro wa kweli na wa ajabu wa Ufalme wa Mungu ukitawala katika siku zetu.

Lakini hata ingawa kwa wakati huu na katika ufalme huu wa kiroho sisi tunaendelea kufurahia amani inayopatikana maishani mwetu kuititia kwa Yesu Kristo, tungali tunatarajia kwa hamu na ghamu kuu wakati ambapo tutakuwa Mbinguni kwenye uwepo wa Mungu.

—mws



JE, WAJUA?

Andiko: “... wana wa Mungu waliwaona hao binti za wanadamu ya kuwa ni wazuri; wakajitwalia wake wo wote waliowachagua” (Mwanzo 6:2).

Kipindi: Kabla ya Mungu kuangamiza ulimwengu wakati wa Nuhu.

Wana wa Mungu: Uzao wa Sethi na wengine ambao walikuwa wamemduisha Mungu katika ufahamu na ibada zao na ambao walikuwa wenye tabia za kitauiwa.

Binti za wanadamu: Uzao wa Kaini na wengine ambao walikuwa wamemwacha Mungu na kufuata njia za kimwili.

Fundisho: Mkristo akimwoa mtu asiye Mkristo mwisho wake ni watu kudhoofika katika mambo ya kiroho.



Nikaapo Gizani

“...nikaapo gizani, Bwana atakuwa nuru kwangu” (Mika 7:8).

Katika nyakati hizi zetu ambazo zina giza nyingi Bwana atashuka na kupanya katika gizo hilo kwa mwangaza wake wa upendo na kwa ukweli wake. Katika siku zilizoja uchungu mwingu wa kimwili, masumbufo ya kiakili, au moyo wenye kuuma, Bwana atatuzungukia kwa usalama wake na tutafahamu kwamba Yeye anatujali na kwamba hata wema wake utatuponya.

Kunaweza kufika wakati ambapo wewe unajihisi kwamba umo gizani—huendi mbele wala nyuma. Hata ingawa siku zako za usoni zinaonekana kuwa na giza kuu, na yatakayojiri katika siku hizo huyajui, kuna amani ambayo mtu hupata wakati anatalia katika mwanga wa Bwana Yesu. Ni katika mwanga huo ndipo tunaweza kupata ujasiri na nguvu za kuikelele siku ijayo. Shauku la Bwana ni kwamba wewe uje kwake na udumu naye ili akuletee mwangaza unaotokana kwake wakati umekubali kwamba upendo wake kwako ni wa milele. Ulimwengu wenyewe umo gizani na giza lake linazidi kuwa kubwa, lakini ukweli wa Neno la Mungu, ambao utadumu milele, utatuletea miali ya mwanga ambayo inatuonyesha njia ya kutorokea ili tutoke humo gizani.



Hata ingawa ulimwengu unaonekana kuwa usio na tumaini lolote, na hata ingawa hali za maisha yako zinaonekana kujaa giza totoro, Yesu alifika ulimwenguni ili atuletee tumaini inayofika hata mahali ambapo watu wamekata tamaa. Hatuna haja ya kukaa gizani kwa kipindi cha muda mrefu kwa maana Rafiki na Mwokozi Wetu Yesu Kristo anakuja na atatuletea mwanga na furaha miyoni mwetu, miyo ambayo sasa imejaa uzito mwingu.

UTAKATIFU KWA BWANA